# Mikakati ya Kuhakikisha Udhibiti wa COVID-19 kwa viwanda vya chakula

Hati hii inaelezea orodha ya rasimu ya utekelezaji wa mikakati wa kudhibiti hatari ya COVID-19 kwa kampuni za chakula. Hatua zinazoweza kutekelezwa zimepangwa kufuatia kanuni ya "TOP"(Technical, organizational, professional) – yaani Kitaalam, Kishirika na pia Kitaaluma. Huu ni mwongozo tu na kampuni yoyote inayopewa inahimizwa sana kurekebisha hii ili iwe sawa na hali zao halisi. Hii ni kazi inayoendelea; tafadhali wasiliana na mwenyekiti ikiwa unayo maoni ya marekebisho. Tutachapisha toleo zilizosasishwa tunapoendelea kuboresha hati hii.

## Mikakati ya Kitaalamu

- ☐ Weka vituo vya kunawa mikono haswa mahali pa kuingia na kutoka kwenye majengo.
- ☐ Dhibitisha kuwa sabuni unayotumia inauwezo wa kukabiliana na virusi
- ☐ Tathmini usambazaji wa glavu, barakoa na mavazi mengine ya kukinga mwili, zingatia matumizi mema kwa viwango vinavyokubalika na pia kuwa wa kuagiza upya vifaa hitajika kwa wakati ufaao bila kupitisha viwango vinavyohitajika
- ☐ Tathmini usambazaji wa vifaa vya kusafisha, vidhibiti sanifu, zingatia matumizi mema kwa viwango vinavyokubalika na pia kuwa wa kuagiza upya vifaa hitajika kwa wakati ufaao bila kupitisha viwango vinavyohitajika
- ☐ Tumia alama sahihi inayopitisha jumbe na kuelekeza tabia za kupunguza hatari ya kuadhirika na ugonjwa wa Covid-19 kwa wafanyikazi

  Mifano:

  - ☐ Taratibu ya kuosha mikono
  - ☐ Matumizi ya glavu
  - ☐ Kuvalia barakoa
  - ☐ Kusafisha/kunawa kutumia sabuni na kemikali zinaweza kuuwa virusi
  - ☐ Dalili za COVID-19 na mikakati ya kudhibiti usambazaji
- ☐ Tambua maeneo yaliyo na hatari kwa mfano nyuso za vilivyomo katika mazingira na kisha kuza utaratibu wa kusafisha mazingira hayo na pia kuwa na cheti kinachoaschashria kuwa maeneo hayo yanasafishwa hadi yakangara mara kwa mara

## Mikakati ya Kishiriki

- ☐ Teuwa mtu mwenye uwezo na ukakamavu ili kushughulikia mawasiliano na uratibu wa ugwonjwa wa COVID-19.
- ☐ Panga mikutano ya wafanyakazi juu ya mikakati ya kudhibiti COVID-19 (kutii umbali wa kijamii wakati wa mikutano hii, treni kwa vikundi vidogo na uweke umbali wa Zaidi ya futi sita kati ya watu) na usasishe mara kwa mara na ukumbushe wafanyikazi juu ya mikakati ya udhibiti wa COVID-19. Tumia mikutano hiyo kutilia mkazo hoja hizi na kuwasiliana na

- ☐ Tekeleza sera ya kuwapa waliowagonjwa ruhusa ya kupumzika na kutokuja kazini
- ☐ Kuwa na njia ya kuripoti kwa siri magonjwa wa kibinafsi na mawasiliano ya karibu na watu wanadhibitishwa kupatikana na ugonjwa wa COVID-19

☐ Punguza idadi ya wafanyikazi kwa kiwango cha chini kinachohitajika ili kufanya operesheni iendelee wakati wa kutekeleza umbali wa futi sita baina ya wafanyikazi

☐ Panga wafanyakazi katika vikundi wakati wa mabadiliko ili kukuza njia za kudumisha umbali ufaao kati ya watu wakati wa kazi na mapumziko

☐ Chagua mtu au timu ndani ya shirika kusafisha mara kwa mara na dawa ya nyuso zilizoguswa mara kwa mara ili kudhibiti virusi kwenye nyuso za mazingara

☐ Zuia wageni wasio wa dharura na wanakandarasi wa nje ambao sio lazima waingie kwenye kituo

☐ Zuia utengamano na madereva wa lori na pia punguza harakati zao kwenye kituo

☐ Tambua usambazaji wa bidhaa ambao unaweza kuhatarishwa katika mnyororo wa usambazaji wa sasa na ugawaji wa mpango ipasavyo.

☐ Ikiwa wakati wowote kuna badala au mabadiliko katika utengenezaji au ufungaji wa vyakula, mpango wako wa usalama wa chakula unapaswa kukaguliwa; hii inaweza kusababisha hitaji la ukaguzi wa mamlaka ya mchakato.

☐ Tekeleza utaratibu wa kawaida wa kufanya kazi unaolezea hatua zinazopaswa kuchukuliwa ikiwa mfanyikazi amepimwa kwa COVID-19 na /au amepatikana kuwa na COVID-19

---

## Mikakati ya Wafanyikazi

☐ Endeleza na kutumia itifaki ya uchunguzi wa wafanyikazi kwa mfano

- ☐ Ni vyema kuwa na njia za kukagua dalili zozote za covid kwa kuweka recodi ya kijumla
- ☐ Nakili orodha ya dalili za COVID-19 zitakazotumika kuchunguza wafanyikazi

☐ Waelezee wafanyikazi kuzingatia umbali kati yao kwa

- ☐ Kuwa Umbli wa angalau futi sita kila wakati
- ☐ Kuepuka migusano kati yao kwa mfano wasisalmiane kwa mikono
- ☐ Funika mdomo na mapua kwa kutumi barakoa iwapo umbali huu hautawezekana

☐ Fanya kuboresha upya maarifa ya wafanyakazi juu ya usafi sahihi wa mikono, pamoja na mazoea ya kuvalia glavu, kunawa mikono na kujiepusha na kugusa nyuso zao

☐ Tengeneza na kutumia itifaki ya usafi wa pumzi kama dalili ya uwepo wa Covid-19

☐ Zingatia na kukuza tabia za kukinga maambukizi kama vile kubadilisha tabia, kwa mfano, watu kunawa mikono na kutogusa ncha ya milango

☐ Weka vizuizi dhabiti katika vyumba vya mikutano ili kudumisha umbali ufaaao kati ya watu walio katika chumba.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE · PURDUE UNIVERSITY · Cornell University

*This document is made possible by the generous support of the American people through the United States Agency of International Development (USAID). The contents are the responsibility of the authors and do not necessarily reflect the views of USAID or the United States Government. Program activities are funded by USAID under Cooperative Agreement No. 7200AA19LE00003. This document was updated on August 26, 2020.*